

## AJABU YA MUZIKI: Kutumia Muziki wa Hip-Hop ili Kuimarisha Ustadi wa Kusoma na Kuandika wa Wanafunzi katika shule ya Marbut Traditional Theme School

Huku muziki wa hip-hop ukiadhimisha miaka 50 tangu kuanzishwa, wanafunzi wengi hufurahia kusikiliza hip-hop ya kisasa lakini hawana ujuzi kuhusu historia ya uanzilishi wake. Andre Mountain, mwalimu mkuu wa Marbut Traditional Theme School, amejitolea kubadilisha hilo na kuimarisha uwezo wa wanafunzi wake wa kusoma na kuandika katika mchakato huo.

Mwalimu mkuu Mountain na timu yake wamefaulu kuanzisha *Maabara ya Kujifunza Hip Hop*, inayofanana na [Maabara ya HipHopEX](#) katika Chuo Kikuu cha Harvard. Ni darasa linalositisiza shughuli zinazotegemea kusoma na kuandika zinazotokana na fasihi ya Waafrika-Wamarekani na masomo yanayozingatia sanaa. Wanafunzi wanasomea uandishi bunifu, masomo ya vitabu na fursa zingine za kielimu ambazo sanaa ya Hip-Hop inaweza kutoa. Lengo kuu la *Maabara ya Kujifunza Hip Hop* ni kuwapa wanafunzi waliohitimu na wa shule ya upili wa eneo jukwaa la kuchunguza na kujaribu uwezo mkubwa wa sanaa ya Hip-Hop katika mazingira mbalimbali ya kielimu.

Maabara ni mahali pazuri pa wanafunzi na walimu kukutana pamoja na kutafakari mada kama vile kusoma na kuandika, utamaduni wa mijini na wa vijana na haki ya jamii. Kama Mwalimu mkuu Mountain alivyoeleza, kwa kuhusika katika majadiliano, kusoma nyenzo zinazofaa, na kubuni sanaa, kila mtu anaweza kufaidika kutokana na uzoefu wa kushirikiana na wa kielimu.

“Hip-hop ni ushairi wa kisasa; ni fasihi, na tunataka kutumia kile kinachowavutia wanafunzi. Wanafunzi wetu wengi wanavutiwa na kupendezwa na utamaduni wa hip-hop,” alisema Mountain. “Kama shule, tunachukulia hii kama fursa ya kuongeza ushiriki wa wanafunzi na kukuza maudhui yaliyo kwenye mtaala. Kwa hivyo, tunajaza mtaala na shughuli ambazo zitafanya wanafunzi wahusike zaidi.”

Maabara hiyo ilianzishwa mwaka jana wanafunzi waliporejea shulenii kufuatia kufungwa kutokana na janga la COVID-19. Wafanyakazi wa shule hiyo walibuni njia mwafaka ya kurejesha upendo wa wanafunzi wa kusoma. Dhana hii ya maabara ilitoa fursa nzuri ya kuboresha ushiriki wa wanafunzi. Kwa msingi huo rahisi, darasa ambalo halikuwa likitumika lilibadilishwa kuwa eneo zuri lililopambwa kwa mabango na kazi ya sanaa inayoshehekewa wasanii wa hip-hop.

“Unapotazama darasa hili, utaona uwakilishi wa utamaduni wa mijini, uzoefu wa Waafrika-Wamarekani kote chumbani,” alisema Mountain. “Na tulitaka kitu kama hicho kwa watoto wetu—maabara ambapo wanaweza kubuni, kufanya makosa, kuwa na majadiliano na mijadala. Sio darasa la kawaida; ni jambo la kipekee katika shule kama hii ya nyanja mahususi za masomo.”

Walimu wanahimizwa watumie fursa hiyo kuwasajili wanafunzi wao kwa ajili ya kutembelea maabara. Wana chaguo la kuongoza somo wenyewe au kuomba msaada wa mwalimu mwingine.

Msaидиzi wa kituo cha habari anapatikana pia kusaidia wanafunzi na mahitaji yao ya kusoma na kuandika. Katika uzoefu huu wote, wanafunzi watapata maarifa muhimu katika historia ya hip-hop na kuboresha uwezo wao wa usanii. Pia wana fursa ya kuchanganua maneno ya nyimbo za wasanii maarufu wa hip-hop kutoka Atlanta, na kutoa fursa ya kina ya kujifunza kupitia sifa za eneo.

“Wasanii wa Atlanta huzungumzia juu ya maswala halisi ya kijamii—maisha ya kijana anayekua katika jiji pana la Atlanta,” Mountain alisema. “Hatutaki tu kuzingatia nyimbo zilizotungwa huko Bronx wakati hip-hop ilipoanza, lakini pia kuzingatia mchango wa Atlanta kwenye utamaduni wa hip-hop.”

Wanafunzi wa gredi ya tano London Christen na Jase Kurtz wanafurahia mada katika *Maabara ya Kujifunza Hip Hop*.

“Ninafurahia kwa sababu tunapata kujifunza zaidi kuhusu muziki wa hip-hop. Unapotafiti maana ya hip-hop, haitakuambia maana halisi,” alisema London. “Lazima ujifunze na usikilize mwenyewe.”

“Ninapenda historia ya Weusi, na Watu Weusi walibuni hip-hop,” alisema Jase. “Kwa hivyo, napenda kuja kwenye maabara. Ninapenda kujifunza kuhusu hip-hop. Ni poa sana.”

Kulingana na Mwalimu mkuu Mountain, maabara inalenga kuhimiza shule zingine kuunda nafasi za kipekee za kujifunzia zinazokuza uvumbuzi na ujifunzaji wa wanafunzi.

“Lengo ni kuhamasisha shule zingine zizingatie mitaala yao na kile ambacho mitaala hio inaweza kufunza,” alisema. “Sio lazima waanzishe maabara ya hip-hop, lakini kitu ambacho kitachochea hamu ya mwanafunzi ya kujitosa zaidi katika masomo wanayojojifunza.”

XXX